

HeRi

Mbabe wa Magonjwa



ULIMWENGU WA MAGONJWA HAT ARISHI UJULIKANAO KAMA MAHA. ULMWENGU AMBAO MAGONJWA HUIJIFICHA.



SHUJAA HERI MBABE WA MAGONJWA KUTOKA KWENYE ULMWENGU WA MASHUJAA MWENYE NGLUVU ZA AJABU ZA KUPAMBANA NA MAGONJWA AKWA TAYARI KWA MASHAMBULIZI.



SISI NDIO MAGONJWA HATARI. SUBIRI TUKLIONYESHE HATARI YETU WEWE DOGO.


HERI NA JENERALI CORONA WANAANGALIANA TAYARI KWA MAPAMBANO.



SIKLOGOPI CORONA,
HATA WEWE MALARIA NA
KIPINDUPINDU.



KIPINDUPINDU, MALARIA NA JENERALI CORONA
WAKIMLIANGALIA HERI KWA HASIRA.



HERI ANAINGIZA MKONO KWENYE LUBEGA YAKE NA KUCHOMOA RUNGU.



HILI RUNGU NI SILAHA YA KUJILINDA NA MAGONJWA, YOTE.



MAHA WAKITIMUA VUMBI KUJA KUMSHAMBULIA HERI,
YEYE ANATULIA KIMYA NA KUWASUBIRI KISHUJAA.



GHAFLA, JENERALI CORONA ANARUKA JUU NA KUTUA KWENYE BEGA LA HERI.






HERI ANADONDOKA CHINI KWA MALMIVU MAKALI.





MAHA WAKADHANI WAMEMSHINDA HERI,
KUMBE ALIKUWA BADO HAJAKUBALI
KUSHINDWA NA MAGONJWA.




HERI AKASIMAMA KISHUJAA NA KUKUNJA NDITA KWA HASIRA.

SIWEZI KUKUBALI
MAGONJWA YANISHINDE NA
YAENDELEE KUWADHURU WATOTO.





VUMBI LINA RUKA HUKU NA KULE, HERI AKIWASHAMBULIA MAHA KIJESHI.




SHUJAA HERI AKAFANIKIWA KUYAANGAMIZA MAGONJWA NA KUWA MSHINDI.



MAHA WAKILUGULIA KIPIGO KIKALI KUTOKA KWA HERI. WAKAJIFICHA NYUMA YA MAWE KWA UOGA NA KUTETEMEKA.



NI ASUBUHI TULIVU KATIKA KIJIKI CHA BUSI,
HII NI SIKU MAALUMU KWA AJILI YA MNADA.



HUYU NI INA
AMBAYE HUPIGA CHAFYA
BILA KUZIBA KINYWA.



HUYU NI SUGE
AMBAYE HANAWI MIKONO
AKITOKA CHOONI.



HUYU NI MUKI
AMBAYE HULALA BILA
CHANDARUA.




MANDHARI YA SHULE YA MSINGI GOGONI, SHULE WANAYOSOMA WATOTO WENGI KATIKA KIJIKI CHA BUSI.



JAMANI LEO NDIO SIKU YA MNADA, INA USISAHAU KUJA NA NGOMA YAKO.




SAWA, LEO TUTACHEZA NGOMA SANA.



HALAFU MUKI TUKITOKA MNADANI NAKULETEA DAFTARI NYUMBANI UANDIKE NOTES.

WOTE WAKIWA TAYARI KWA AJILI YA KUMALIZA MASOMO NA KUELEKEA MNADANI.






WALIANZA KULA MIHOGO YAO BILA KUNAWA MIKONO WAKATI MAJI NA SABUNI YALIKLWEPO.



VIJIDUDU VILIMOYOPO KWENYE MIKONO YAO MICHAFU VIKAAANZA KUTOA TAARIFA KWA KUTUMIA MAWIMBI KUELEKEA ULIMWENGI WA MAHA.



TAARIFA HIZO KUTOKA KWA
VIJIDUDU ZINAMFIKIA
JENERALI CORONA.



KHEE! KUMBE BADO KUNA
WATOTO HAWAJILINDI
NA MAGONJWA?
SUBIRI NIWATAFUTE.



WAKO WAPI HAWA WATOTO
WAZEMBE, WASIONAWA
MIKONO KWA SABUNI.



NDANI YA WODI YA MAHA - KIPINDUPINDU
NA MALARIA WAMELALA KITANDANI.



LISAWA WA KORIDO YA WODI, MLANGO UNAFUNGULIWA NA TUNAONA
KIVULI CHA JENERALI CORONA AKIINGIA WODINI KWA KISHINDO.





MAKAMANDA!
MALARIA, KIPINDUPINDU!



NDIO
JENERALI CORONA.



JENERALI CORONA AKASIMAMA KATIKATI YA VITANDA VYAO KUWAPA MPANGO MIKAKATI.

TAARIFA ZILIZONIFIKIA
NI KWAMBA WATOTO WA
KIJIJI CHA BUSI HAWAJIKINGI
NA MAGONJWA.

SAWA MKUU,
LUTENI KIPINDUPINDI
UNAONAJE TUWAFUATE?

NDIO KAPTENI MALARIA
NI MUDA WA KWENDA
KUWASHAMBULIA,
SIMAMA TWENDE!



TWENDENI!!!!

HAAHAAA
CORONA KAMA
ZOTE.



SASA NI MUDA
WA KUWAAMBUKIZA.



WAKATI NILIOUSUBIRI
SANA UMEWADIA,
TWENDE!

ULIMWENGU WA MASHUJAA.



WAKATI HERI AMASIMAMA KWENYE JWE KUBWA, RUNGU LAKE LIKATINGISHIKA KUMPA TAARIFA YA UJIO WA MAHA.




RUNGU LINALIA
KUASHIRIA MAGONJWA
YAMERUDI. NGOJA
NIKAWALINDE WATOTO.

KHI KHI!!

HERI AKARUKA JULU HEWANI NA KUANZA SAFARI YA KWENDA KUWALINDA WATOTO DHIDI YA MAGONJWA HATARISHI.



WUUSH





WUUSH



MAHA WAKACHUKUWA MTUMBWI NA KUPIGA KASIA HARAKA KUWAHI KUFIKA KIJJI CHA BUSI ILI KUWASHAMBULIA WATOTO WASIOJIKINGA NA MAGONJWA HATARISHI.



PIGA KASIA KWA HARAKA WEWE!!
UMENISIKA KIPINDUPINDU.



NDIO JENERALI CORONA.



NGOJA NIPAE HARAKA,
SITOKUBALI MAGONJWA YAWADHURU
WATOTO WENZANGU.



WAKATI HUO HUO HERI ALIONGEZA KASI ILI AFIKE
KIJJI CHA BUSI KABLA YA MAHA.




MAHA NAO WALIONGEZA KASI ILI WAFIKE
MAPEMA KABLA HERI HAJAWASILI.

MUKI, INA NA SUGE WANATEMBEA, KATIKATI YA KUNDI KUBWA LA WATU.



SHUGHULI ZA MNADANI ZILIKUWA NYINGI, WATU HUKU NA KULE WAKILIZA NA KUNUNUA VITU.






MAHA WAKAWASILI NCHI KAVU WAKIWA NA SHAUKU, JENERALI CORONA NA KIPINDUPINDU WAKATANGULIA KIJIJINI HUKU WAKIMUACHA MALARIA AKIEGESHA MTUMBWI NA KUWEKA NANGA.




MAGONJWA HATARI YAMESHAFIKA KABLA YANGU. NGOJA NIWAHI.



KIPINDUPINDU NA JENERALI CORONA WAKAELEKEA MOJA KWA MOJA MNADANI LAKINI MALARIA ANAONEKANA KUKATIZA NJIA NYINGINE.



TUNAWAONA MUKI, SUGE NA INA WAKIWA SOKONI WAKICHANGANYIKANA NA KUNDI LA WATHU WALIOENDA KWENYE MNADA.



GHAFLA, SHUJAA HERI MBABE WA MAGONJWA ANATUA MBELE YAO NA KUWASALIMIA.

OYO, MPO VIZURI WENZANGU?

HUYU NINAYEMSIKIA ANATUONGELESHA NI NANI?

ATAKUWA NOEGE MTU!

NI MTOTO KAMA SISI, LAKINI AMEVAA KAMA SHUJAA VILE! SIJUI ATAKUWA MALAIKA?




MAMBO VIPI WATOTO WENZANGU?



POA!



SAFI!



NAITWA HERI MBABE WA MAGONJWA NINA WAELEKEZA WATOTO KUJIKINGA NA MAGONJWA.


KUNA MAGONJWA HATARI MATATU MALARIA, KIPINDUPINDU NA CORONA YANAKUJA KUWASHAMBULIA. TUJIANDAE!

JAMANI HERI TUSAIDIE KUPAMBANA NA MALARIA. HASA MUKI ASIYELALA KWENYE NETI.


CORONA!

KIPINDUPINDU NAKIOGOPA. HERI TUSAIDIE TUSIUMWE.

HERI ANAWAVUTA KARIBU WANAKAA KWENYE DUARA
NA KUENZA KUPANGA MPANGO MKAKATI WA KUKABILIANA NA MAHA.




MSIHOFLU, NITAWASIDIA
NA NYIE MUWE WABABE
WA MAGONJWA KAMA MIMI.




SASA TUTAANZA NA MBINU
ZA KUKABILIANA
NA CORONA. MPO TAYARI?

NDIOOOO!



MUKI, INA NA SUGE WAKAUNGANA NA HERI TAYARI KWA AJILI YA KUJIFUNZA KUPAMBANA NA MAGONJWA KUTOKA KWENYE ULIMWENGU WA MAHA.







HERI AKAENDELEA NA HATUA YA PILI YA
KUJIKINGA NA MAHA.



HERI AKAAANZA KUNAWA HUKU WAKIWAPA MAELEKEZO KWA HATUA ZOTE.





HAPANA SUGE, USISHIKE USO KABLA YA KUNAWA UTAJIPAKA VIJIDUDU VYA MAGONJWA.

ASANTE, HIVI ITAKUWAJE KWA WENZETU WANAOSOMA SHULE ZISIZO NA MAJI?




HATA SERIKALI PIA INAZEZA KUTENGENEZA VISIMA NA KUWEKA MABOMBA YA MAJI SAFI.

ITABIDI TUWAOMBE WAZAZI WAWASIDIE KUPATA MAJI NA SABUNI MASHULENI.




EBO! WANAJILINDA. LEO TUNASHINDWA.



WAMESHAJISTUKIA TAYARI WANA NAWA MIKONO!

JENERALI CORONA NA KIPINDUPINDU WANAKATA TAMAA KABISA, WANASHINDWA KUWASHAMBULIA WATOTO KWASABABU WAMEJUA KUJIKINGA.



KUTOKANA NA KUPATA UGUMU WA KUWAAMBUKUZWA WATOTO WANAKASIRIKA SANA. LAKINI WANAPATA WAZO LA NJIA NYINGINE YA KUWASHAMBULIA WATOTO.

WATAJISAHAU TU!
WANAWEZA WAKALA MATUNDA
BILA KUYAOSHA, HII NI
NJIA YETU KUWASHAMBULIA.
TWENDE!

TWENDENI KWENYE NGOMA.

TUMEKUELEWA HERI.
NAFIKIRI ITAKUWA VIZURI
KUWAE LIMISHA WATOTO
WENZETU PIA ILI NAO
WAWAZE KUJIKINGA.

NASHAURI TUSIENDE.
TUEPLIKE MIKUSANYIKO
KUJILINDA NA
CORONA.

NA WAZAZI WETU PIA,
ILI TUWEZE KUJILINDA
NA KUZILINDA FAMILIA ZETU.
JAMANI, UMEONA
YALE MAEMBE!?

TUMEKUELEWA.
KWANINI TUSIWAELIMISHE
WATOTO WENZETU NAO
WAJIFUNZE PIA?

SLIGE ANAKIMBIA GENGENI
KUWANUNULIA MARAFIKI ZAKE
MAEMBE.



ENHEE KIPINDUPINDU
KATEGE KWENYE
MAEMBE,ATAKULA TU
BILA KUOSHA.



SUBIRI NIKAYAPAKAZE
BAKTERIA MAEMBE DODO
YAKE...



KIPINDUPINDU AKARUKA
NA KUJARIBU KUWAHI
MAEMBE.



GHAFLA HERI AKAYAWAHI MAEMBE KUTOKA KWA SUGE ILIYETAKA KULA BILA KUYAOSHA.




MUKI HAPANA!! USILE KWANZA, UNAJUA KUNA BAKTERIA WABAYA WANAOSABABISHA MAGONJWA YA KUHARA? KWANZA UNATAKIWA KUYAOSHA VIZURI MATUNDA KWA MAJI SAFI TIRIRIKA.

HEEEE! HERI ANAYALINDA MAEMBE YANGU!



HERI ANAELEKEA KWENYE NDOO YA MAJI SAFI TIRIRIKA KUONESHA JINSI YA KUOSHA MATUNDA.





BAADA YA KUOSHA,
NDO TUANZE KULA MAEMBE
YETU!

SASA SISI MAGONJWA
TUTA MUAMBUKIZA
NANI KAMA WOTE
MNAJIKINGA.

*MLIKI NA SUGE WAKAAMLIA KUANZA KUELEMISHA WATOTO WENZAO
KUHUSU KUJIKINGA NA MAGONJWA.*



UNAPAKA SABUNI NA
KUSUGUA HUKU NA HUKU.



HII BARAKOA INAVALIWA HIVI,
KUZIBA PUA NA MDOMO.

SUGE NA INA WAANZA KUWAKUMBUSHA WANAKIJIJI
JINSI YA KUJIKINGA NA MAGONJWA.



NYUMBANI KWAO MUKI



MALARIA AKIWA NA MBU WAKE WAKITEGA NA KUSUBIRI DIRISHANI, CHUMBANI KWA MUKI.

KAENI TAYARI MBU WANGU.


HAINA SHIDA MALARIA.


NIKO TAYARI.

SINDANO NIMEIKOKI.

MARA GHAFLA MLANGO UNAFUNGULIWA, HERI, MUKI NA MAMA YAKE WANAINGIA CHUMBANI.

BAADA YA KUWASHA TAA, WANAJIANDAA
KUPULIZA DAWA YA KUUHA MBU NDANI YA NYUMBA.





LINAONA MAMA
MBU WAMESHAINGIA.
TUPULIZE
DAWA NA TULALE
NDANI YA NETI

VIZURI SANA MUKI.
HAYA WAPULIZIE MBU
WOTE NA UTANDIKE
CHANDARUA VIZURI.



NINAFURAHU SANA
KIUNA WAZAZI NA WATOTO
TUNAJILINDA
NA MAGONJWA!


HERI NA MUKI WAKAANZA
KUPULIZA DAWA KWA UMAKINI
NDANI YA NYUMBA.




LIKAFIKA MUDA WA HERI KUONDOKA
KURUDI KWENYE ULIMWENGI WA MASHUJAA.

SAWA. WASALIMIE
HUKO NYUMBANI KWA
WABABE.

MIMI NAONDOKA,
ENDELEENI KUWAFUNDISHA WATOTO
WENGINE JINSI YA KUJIKINGA
NA MAGONJWA.



HERI AKARUKAA JUU SANA NA KUANGALIA KIJIKI
CHA BUSI NA KUAMINI AMEKIACHA SALAMA. WAKATI
HUO HUO MUKI, SUGE NA INA WALIKUWA
WAKIMUANGALIA KUPITIA DIRISHANI.





HeRi

Mbabe wa Magonjwa

KITABU HIKI KIMETENGENEZWA NA ADD INTERNATIONAL KWA AJILI YA WATOTO KUJIFUNZA NA KUELEWA ZAIDI JULU YA MAGONJWA HATARI, ILI WAISHI SALAMA. WATOTO WAKISOMA KITABU HIKI, WATAJUA MBINU ZA KUJILINDA NA KUWA WABABE WA MAGONJWA.

WATOTO NI TAIFA LA LEO, WAJILINDE NA MAGONJWA.

*HADITHI NA MICHORO
IMEFANYWA NA:*



